

**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)**  
**MKATABA WA KAZI YA KULETA VIFAA VYA UJENZI AMBAVYO NI MCHANGA NA KOKOTO**

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 25 mwezi 05, 2022

**KATI YA**

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha Mikumi S.L.P. 110 ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 2849 Dar es Salaam (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

**NA**

GOMBE PERTTY GROUP, S.L.P. 22, MAHENGE - ULANGA (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama mzabuni") kwa upande mwingine.

KWA KUWA Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Ulanga;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Ulanga;

KWA KUWA Mwajiri amefanya majadiliano na "Mzabuni" kwa shilingi 3,720,000/= kwa ajili ya kuleta vifaa vya ujenzi eneo la ujenzi kwa Mgawanyo ufuatao:-

S/N	JINA LA kazi	KAZI KUFANYIKA	ZINAZOTAKIWA	GHARAMA KWA KILA KAZI	GHARAMA YA JUMLA KWA JENGO
1.	KOKOTO NA MCHANGA	a. Kuleta kokoto ½" mita za ujazo 20@90,000/= b. Kuleta mchanga mita za ujazo 80@24,000/=		1,800,000/= 1,920,000/=	3,720,000/=
<b>JUMLA KUU</b>					3,720,000/=

NA KWA KUWA Mwajiri amepatia Mzabuni maelekezo ya muda ambao vifaa vya Ujenzi (*Schedule of materials*) vitahitajika eneo la ujenzi.

**HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:**

**1. GHARAMA YA UFUNDI**

Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania 3,720,000/=, Mzabuni atafanya kazi ya Kufanya kazi ya kuweka kuleta Kokoto na Mchanga Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama "Gharama ya Uzabuni"

**2. MABADILIKO YA GHARAMA YA UJENZI (CONTRACT SUM ADJUSTMENT)**

Gharama ya uzabuni haitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri.

**3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO**

Mwajiri atamlipa Mzabuni kwa hundi ndani ya siku kumi na nne baada ya kuleta vifaa vyote vya ujenzi kwa ujumla wake na baada ya kuidhinishiwa malipo na wasimamizi wa site

**4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUAHIRISHA KAZI**

(a) Mzabuni atakabidhiwa eneo la tarehe 28 mwezi 05 2022 au tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa. Iwapo Fundi atakabidhiwa tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa, pande zote zitaweka kumbukumbu kwa maandishi siku ya makabidhiano ambapo pande zote mbili zitasaini.

(b) Mzabuni atakamilisha kazi ndani ya siku 30 toka tarehe ya makabidhiano ya kazi hiyo. Iwapo kutatokea mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri, siku ya ukamilishaji wa ujenzi inaweza kubadilika.

(c) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Fundi kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo.

**5. WAJIBU WA MZABUNI**

Mzabuni atakuwa na wajibu ufuatao: -

(a) Kuleta vifaa kwa wakati kama inayotakiwa (*Schedule of materials*) sambamba na maelekezo ya Mwajiri;

(b) Mzabuni atatakiwa kufanya kazi kwa mpango kama atakavyoongozwa na mpango kazi atakaopewa na wasimamizi wa site.

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA  
MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA VETA  
MIKUMI

Jina: Marynancy Kazosi Saini: Mogoso

Wadhifa: Mkuu wa Chuo Tarehe: 25/05/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: LADISLAUS P. KALATUNGA Saini: [Signature]

Wadhifa: Msimamizi, Wamuruzi Tarehe: 25/05/2022

IMESAINIWA NA FUNDI

Jina: FURAHX LILONGERI Saini: [Signature]

Wadhifa: MURUGENZI Tarehe: 25/05/2022



Mbele ya (Shahidi)

Jina: NOVATIUS MXYIJI Saini: [Signature]

Wadhifa: msimamizi Tarehe: 25/05/2022